HALMASHAURI YA WILAYA YASENGEREMA

Tarehe: **04 Septemba, 2019**

TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI Na: LGA/094/HQ/2019-2020/NCS/03
Lot A1,A2,A3,B,C,D,E,F,G,&H

ZABUNI YA UWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA-KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

1.Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema katika kuboresha ukusanyaji wa mapato yake ya ndani kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 itaendelea kuwatumia mawakala ambao watakusanya mapato hayo kwa niaba ya Halmashauri ya wilaya.

2.Halmashauri inatangaza zabuni ya kukusanya mapato ya ndani kwa mtu binafsi,kundi la watu lililosajiriwa kisheria,Taasisi zisizo za kiserikali au kampuni yenye uwezo na uzoefu wa kukusanya mapato.

3.Maeneo ya kukusanya mapato yaliyoko ndani ya Halmashauri ya wilaya ya Sengerema yanayotangazwa ni kama ifuatavyo:-

SEHEMU A: USHURU WA MIALO YA SAMAKI

A1.Kijiweni-Chifunfu,Lyakanyasi,Biswa,Nyazune,Juma kisiwani,Kasenyi,Lugongo,Nyamazugo na Bungonya.

A2.Katunguru, Kasomeko,Karumo,Chamabanda,Igalagalilo,Kamanga,Irunda na Nyarwambu.

A3.Kahumulo,Busisi,Lubanda,Nyamasale,Igeye,Mulaga,Buyegu,Chikomelo,Ma bilu na Kaningu.

SEHEMU B:USHURU WA MINADA
B.Mnada wa Ng'ombe Sima, Minada ya Mbuzi (Sima,Nyanzumla,Nyampande,Lusikwi na Ibondo)

SEHEMU C: ADA YA USAFI MASOKO YA KAWAIDA.
Busisi,Kahumulo,Nyanzumula,Nyanchenche,Buyagu,Mulaga,Kariakoo, Nyamatongo,Kamanga,Karumo,Nyamazugo,Nyamizeze,Bungonya,Mwaliga, Kijiweni,Bihira, Kasungamile,Nyamililo,Nyampande,Tabaruka,Nyasenga. SokoMigombani,SokoMnadani-Nyampulukano,Ibisabageni,Mwabaluhi Tunyenye,Kishinda,Sima,Igaka,Ikoni,Iyogelo,Buzilasoga,Kanyelele,Katunguru,L usikwi,Ilunda,Ilekanilo,Nyakahako,Lugongo,Mbalagane,Kasenyi,Igalagalilo, Chamabanda,Ngoma 'A'-Igalula,SengeremaMjini-Sokokuu,Misheni.

SEHEMU D:USHURU WA HUDUMA YA VYOO
- Choo Stendi kuu ya mabasi Sengerema,
- Choo Soko la Migombani.
- Choo uwanja wa Mnadani.
- Choo Stendi ya Mwembeyanga.
- Choo Soko Kuu
- Choo cha soko Misheni
- Choo cha soko Kisimacha Chumvi-Nyatukala

SEHEMU E:USHURU WA MADINI YA UJENZI
Madini ya ujenzi ndani ya Halmashauri ya wilaya Sengerema(Mawe,Mcha nga,kokoto,Moramu nk)

SEHEMU F:USHURU WA MAZAO
Mashine za Kukoboampunga Nyatukala na Bukala

SEHEMU G:USHURU WA STENDI NA MAEGESHO
Stendi Kuu, Stendi Mwembeyanga na Maegesho.

SEHEMU H:ADA YA USAFI MACHINJIO-NYATUKALA

Masharti ya zabuni ya Uwakala.
1. Mwombaji awe, mtu binafsi, kundi la watu, Taasisi zisizo za Kiserikaliau Kampuni iliyosajiliwa kisheria.
2. Awe na Leseni ya biashara.
3. Awe na usajili wa mlipa kodi TRA –TIN Namba.
4. Awe na ofisi ya kudumu na ataje mahali inapopatikana na Anuani inayotambulika pamoja na njia za mawasiliano.
5. Mwombaji atalipia ada ya maombi isiyorejeshwa kwa kila 'Lot' atakayoomba kwa kila Kundi kama ilivyobainishwa hapo juu.

6. Nyaraka za zabuni zinapatikana kwa Katibu wa bodi ya zabuni baada ya kulipia ada ya zabuni (Tender fee) ambayo haitarejeshwa.
7. Maombi yote yatatumia nyaraka zilizotolewa na Halmashauri na si vinginevyo. Maombi ambayo hayatafuata masharti ya zabuni yatakataliwa katika hatua ya tathmini.
8. Kila mwombaji ataambatanishamchanganuo wa mapato kwa kila eneo atakaloomba na kubainisha kiwango cha mapato atakachowasilisha katika Halmashauri, kiwango ambacho kitadumu kwa kipindi chote chauzabuni na si vinginevyo.
9. Mwombaji anaruhusiwa kuomba fungu (Lot) yoyote kwenye kifurushi (package) ili mradi alipie ada ya maombi kwa kila lotatakayoomba.
10. Wakala atarejeshewa asilimia 20 hadi 25 **(20%-25%)** ya makusanyo yake ya mwezi kila Mwezi,hivyo mwombaji atatakiwa kufanya utafiti wa kina na kujiridhisha juu ya mapato ya chanzo atakachoomba.
11. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 18/09/2019 siku ya Jumatano saa 4.00 asubuhi na ufunguzi utafanyika mara tu baada ya muda wa mwisho siku ya Jumatano saa 4.00 asubuhi. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanakaribishwa kuhudhuria siku ya ufunguzi.
12. Maombi ya Uwakalayafungashwe pamoja na viambatisho:-

    Nakala (Vivuli) vya;
    (i) Cheti chamlipa kodi TIN Namba.
    (ii) Leseni ya biashara.
    (iii) Stakabadhi ya ada ya maombi ya zabuni.
    (iv) Kitambulisho cha NIDA au Mpiga kura.
13. Maombi yawe nakala halisi moja na nakala kivuli moja yafungwe kwenye bahasha isiyo na utambulisho wa mwombaji na juu ya bahasha iandikwe**Na. ya zabuni, Lot Na. na Maelezo ya zabuni** na kutumwa kwa**:-**

KATIBU,
BODI YA ZABUNI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA
S.L.P 175
SENGEREMA.

14. Maombi yote yatatumia nyaraka za zabuni zinazopatikana kwenye ofisi ya katibu wa bodi ya zabuni baada ya kulipia ada ya maombi.

15. Mwombaji atakayefanikiwa kupata zabuni ni sharti awasilishe malipo ya dhamana ya miezi miwili (2) katika kipindi kisichozidi siku saba (7)baada ya kukabidhiwa barua ya uteuzi wake.Fedhaitalipwa kwenye akaunti ya Amana namba 31601200129(MiscelleneousDepositAccount).Iwapo mwombaji atashindwa kuzingatia sharti hili basi mwajiri atakuwa na mamlaka ya kumpatia mwombaji mwingine bila kumtaarifu mwombaji aliyeshinda.

16.Mwombaji atatakiwa kumiliki na kutumia mashine ya kutolea risiti ya kieletroniki (POS-Point Of Sale Divice Machines) katika kukusanya mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema

17.Gharama za usafi wa mazingira ya chanzo pamoja na karatasi za kutolea Risiti (Rolla) zitakuwa juu ya Wakala mwenyewe

18.Mwombaji atatakiwa kulipa fedha za makusanyo benki kila siku baada ya kupata namba ya kulipia mapato ya Serikali (Control Number) kutoka kitengo cha mapato cha Halmashauri.

19. Mwombaji atatakiwa kulipa ada ya maombi ya zabuni kwa kila kundi(Lot) Tsh.**100,000/=** ambayo haitarejeshwa katika makundi A1,A2,A3,B,C,D,E,F,G & H

Mkurugenzi Mtendaji (W)
SENGEREMA